Usalama wa familia yako na Mtoto wako

JAMII SALAMA KWA WATOTO

Serikali ya Australia inafikiria kwamba watoto ni wa familia zao na ndio mazingira bora kwao kukua.

Serikali inaamini kwamba wazazi wana haki ya kufanya uamuzi kuhusu kulea watoto wao bila kusumbuliwa, mradi watoto wao wanalindwa kutokana na madhara na wanawekwa salama.

Wakati mwingine serikali huhusika na familia na hata pengine huhitaji kuondoa watoto kutoka nyumbani. Idara hii inaitwa Idara ya Huduma ya Jamii Salama kwa Mtoto mara nyingi hujulikana kama “idara” au “Usalama wa Mtoto”. Kazi yao ni kulinda watoto huko Queensland kutokana na kuadhirika.

Familia kutoka asili za wakimbizi zinaweza kuwa na hoja kuhusu sheria za ulinzi wa mtoto nchini Australia. Kwa urahisi hii ni kwasababu ni wazo jipya kwa wengi wao. Ni vigumu kuelewa kwanini serikali inaweza kuhusika na maswala ya familia yao.

Sheria inasema wakati Ofisi ya Usalama wa Mtoto inapokea ripoti kwamba mtoto anaweza kuwa aliumizwa au yuko katika hatari ya madhara, lazima ihusike.

Sheria hizi ni za kila mtu sio tu za jamii za wakimbizi.

Ripoti zinaweza kujulishwa wa mtu yeyote aliye na wasiwasi, pamoja na mwalimu wa mtoto, jirani, rafiki au jamaa. Ndani ya Queensland, baadhi ya wataalam kama madaktari, waalimu, na wauguzi lazima waripoti kesi za madhara zinazoshukiwa kwa Usalama wa Mtoto.

Ikiwa ripoti hii itafanywa kuhusu mtoto wako, afisa wa Usalama wa Mtoto atachunguza ripoti hiyo kwa kuzungumza na wewe, watoto wako/au washiriki wengine wa familia ili kujua ikiwa mtoto wako aliumizwa, alikuwa katika hatari au hakutunzwa inavyotakikana.

Inaeleweka kwako kuwa na hofu au kukasirika wakati mtu wa nje anakuambia cha kufanya kwa watoto wako. Ni muhimu kutulia na kujaribu kuelewa hali ya hoja hiyo. Ni haki yako kuitisha mtafsiri. Wakati wote uombe ushauri wa kisheria kila mara na usitie sahihi kitu chochote ikiwa hauelewi.

Ikiwa Usalama wa Mtoto inaamini kwamba mtoto wako hayuko katika hatari na kwa msaada kidogo, hoja zinaweza kutatuliwa, wanaweza kuunganisha familia yako na huduma zingine za msaada na ushauri. Hii itakusaidia kujua njia mpya za kushughulika na mtoto wako.

Afisa wa Usalama wa Mtoto anaweza kupanga kuwasiliana nawe mara kwa mara au kukutembelea nyumbani na atarekodi kuendelea kwako. Wakati wasiwasi wote umepotea, Usalama wa Mtoto hautahusika tena.

Ikiwa Usalama wa Mtoto inaamini kwamba mahitaji ya mtoto wako hayawezi kutimizwa wakati anaishi nyumbani, watoto wanaweza basi kuondolewa kutoka nyumbani mwako kwa muda mfupi. Usalama wa Mtoto itajaribu kuweka mtoto wako na washiriki wengine wa familia ambapo inawezekana.

Ikiwa watoto wako watalindwa na familia nyingine, ni muhimu kwako kuwasiliana na watoto wako. Unahitaji kuendelea kuzungumza na Usalama wa Mtoto pia na kuhudhuria mikutano iliyopangwa nao.

Wakati unapohudhuria mikutano hiyo unaweza kumpeleka rafiki au mfanyikazi wako wa kesi na wewe kama mtu wa msaada.

Ikiwa Usalama wa Mtoto itahusika katika familia yako:

- Omba upate mtafsiri kila wakati
- Jua kwanini Huduma za Usalama wa Mtoto inajali kuhusu mtoto wako na uliza habari hii kwa kuandika
- Tafuta msaada kutoka kwa huduma za kisheria
- Usiwahi kutia sahihi kwa fomu zozote bila kuzielewa.
- Hakikisha kwamba una mtu wa msaada wakati unapohudhuria mikutano hiyo.
- Wasiliana na watoto wako
- Ikiwa haukubaliani na uamuzi wa Usalama wa Mtoto, zungumza. Unaweza kuomba uamuzi wako kukaguliwa rasmi.
- Weka malalamiko rasmi ikiwa haujatosheka na Usalama wa Mtoto kushughulikia kesi yako.
- Ni hekima kuuliza habari yoyote kwa kuandika. Hii hukupa nafasi ya kutafuta mtu mwingine baadaye, ambaye anaweza kukufafanulia kinachotendeka na ni kwanini.

Watoto wote wanastahili utoto salama, wenye afya na furaha.

Hapa kuna baadhi ya mahali unapoweza kuomba msaada:

- **Huduma ya Mtafsiri wa Simu (TIS) Simu ya Kitaifa**
  131 450
  Huduma ya kutafsiri inapatikana masaa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki.
- **Idara ya Huduma za Jamii za Usalama wa Mtoto**
  1800 811 810 / Baada ya masaa ya kazi 1800 177 135
  Hujibu kwa watu walio na hoja kuhusu maswala ya ulinzi wa mtoto
- **Msaada wa Kisheria Queensland**
  1300 65 11 88
  Hutoa habari ya bure ya kisheria, ushauri na uwakili.
- **Huduma za Kisheria za Wanawake**
  (07) 3392 0670 or 1800 677 278
  Kituo cha kisheria cha jamii kwa wanawake. Wanafafanua sheria na kinachotendeka kortini kwenye maswala mengi ya kisheria na kurejea mashirika mengine ya msaada au mawakili wengine wa kibinafsi.
- **Huduma ya Kisheria ya Wakimbizi na Uhamiaji**
  (07) 3846 3189
  Msaada wa bure katika kesi za uhamiaji na wakimbizi.
- **Laini ya Wazazi**
  (07) 3858 5371 au 1300 30 1300 (8am – 10pm, saa mbili asubuhi hadi saa nne usiku, siku 7)
  Huduma ya ushauri wa simu ambayo husaidia watu kukuza mikakati kuhusu hoja ambazo wazazi wanazo.
- **Mpango wa Queensland wa Kuwasaidia Wahasiriwa wa Mateso na Dhiki (QPASTT)**
  (07) 3391 6677
  Mipango ya kusaidia familia zilizo na mizozo ya kizazi na kitamaduni kupitia ushauri, vikundi na habari.

MDA Multicultural Development Association

This document was developed by Multicultural Development Association (MDA) with funding from the Australian Government Department of Families, Housing, Community Services and Indigenous Affairs (FaHCSIA)